

MTAWALA

FIKRA

CHANYA

MPYA

KUHUSU MWANDISHI



Sir. Peter Fabian N. ni Mwalimu, mtalaamu wa sayansi ya jamii na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Mwandishi anayo elimu ngazi ya shahada katika sayansi ya jamii (Sosholojia) kutoka chuo kikuu cha Dodoma mwaka 2019, stahhada katika maendeleo ya jamii na cheti katika maendeleo na ustawi wa jamii .

Mwandishi ni mtu aliyefanya tafiti mbalimbali ambazo hazijachapishwa, na tafiti hizo zimefanyika kwa kuzingatia vigezo vingine vyote vya utafiti. Pia mwandishi ni mtu anaetoa usaidizi wa masuala mbalimbali ya kijamii hasa kwa wazee waliostaafu na kupoteza stahiki zao kutoka mifuko ya hifadhi ya jamii.

Sir. Peter anao utaalamu na upendeleo wa kipekee katika masual ya siasa, uandishi na diplomasia ya uchumi wa kimataifa..

Sir. Peter amekuwa kiongozi katika ngazi mbalimbali kuanzia shuleni, ni kiongozi wa wizara ya elimu katika shirikisho la wanafunzi wa sosholojia, Kiongozi wa darasa (CR) kwa muda wote wa stahhada.. Pia Sir Peter alishagombea Urais wa serikali ya wanafunzi chuoni bila mafanikio.

Mwisho, Sir Peter ni mwanafunzi bora (Best student) idara ya Sosholojia mwaka wa kwanza hadi wa tatu 2019, na kwa sasa anaendelea kusaidia na kutoa ushauri mbalimbali katika jamii.

DIWANI YA

MTAWALA

Sir. Peter Fabian N.

Imehifadhiwa na Sir.Peter Fabian N. na ni marufuku kudurufu au kunakili kitabu hiki

kwa namna yeyote ile isipokuwa kwa idhini maalumu.

Toleo la Kwanza

TABARUKU.

Ninayatabaruku mashairi haya katika muktadha tofauti tofauti, kwanza kabisa ninajishukuru mwenyewe kwakutumia muda wangu wa ziada na maarifa niliyopewa na mungu kuandika kazi hii yenye lengo la kuuamsha umma wa WaTanzania wa ngazi zote.

Pili, Ninatabaruku Diwani hii kwa wasomaji wote watakaochukua muda wao kusoma mashairi haya yatakayowapa umahiri na uamsho wa kimaendeleo.

Tatu, ninatabaruku kitabu hiki kwa familia yangu na kwa kipekee Mwl. Mandago Mboje Mpamwa kwa ushauri wake.

YALIYOMO.

DIBAJI

WANAFANYA MAKUSUDI

HANA UTOFAUTI

KAZI IENDELEE

MZINGUAJI

TAIFA MNADANI

NYAUUUUUUUU

GIZA

HISTORIA

MAKALIO SAKAFUNI

SERA

USHAURI

TAMAA

SHIBE

TUWABISHIE

NYEGERE

TOKENI USINGIZINI

NAFASI

NINI KIMETOKEA

MATAJIRI FURAHANI

WASHANGILIAJI

MIHIMILI BANDIA

KUTI LA MAZOEA

SALAMU

TUONGEZE UMAKINI

SHATI KUBWA

RUWASA

MAJI

JAMII

MENO YA TEMBO

WAJINGA SISI

MAMBA

KUSINI

NANI

DIBAJI

Mambo mawili ndio yaliyonipelekea kuandika mashairi haya ya Mtawala.

*Kwanza, Nimeshuhudia mambo mengi yaliyotokea nchini tangu uhuru na
kwa hakika nimesuumwa kuandika mashairi haya kwa lengo kuu la
kuonesha jamii juu ya mateso na shida wanazopitia wananchi wa karibu
duniani kote hasa Afrika.. Diwani hii inachora picha halisi ya unyonyaji na
kutokujali kwa viongozi juu ya maendeleo ya wananchi katika nyanja zote.*

*Pili, Diwani hii imeandikwa kwa lengo la kuwakumbusha wanasiasa na
watawala kuwa neno lenyewe mtawala si zuri kwao kuitwa, bali wapaswa
kutenda mazuri yatakayowafanya kuitwa viongozi na si watawala.*

UTANGULIZI.

Mtawala ni mjumuiko wa mashairi ya kipindi kuanzia zama ngumu zenye kugusa maisha ya watu wa Afrika kwa muda wa kuanzia miaka ya 2015 hadi leo. Kitabu hii kinaonesha athari za utawala badala ya uongozi kitu ambacho wananchi wengi wanakikosa katika bara la Afrika.

Mshairi anaeleza kufuatia bahari mbalimbali za kiswahili. Mashairi ya mtawala yameandikwa kwa hisia za ushairi kuonesha yanayojiri katika jamii.

SHUKRANI.

Kwa wasomaji wote.

WANAFANYA MAKUSUDI.

Angalia Sura zao,Uongo umewajaa,
Viongozi Gari zao,Furaha imewajaa,
Pesa,Nyumba vyote vyao,Ajira zina Mawaa,
Wanafanya makusudi,Umasikini kwao mtaji.

Mtazameni malkia,Haeleweki lakini,
Madege Anatumia,,Wananchi Masikini,
Ahadi hajatatua,Kutwa kucha Mawinguni,
Wanafanya makusudi,Umasikini kwao Mtaji.